

## **Injiili Ni Nini ?**

Injili ni hadithi. Ni hadithi ya Mungu. Marko 1:14 = inatuambia Yesu alivyotoka katika majaribu yake huko jangwani, “Akihubiri Injili ya Mungu”

Mathayo 4:23, Inatueleza Yesu alikuja akihubiri “Injili ya Ufalme.” Tazama Mathayo. 9:35; na Mathayo. 24:14.

1<sup>st</sup> Wakorintho 15:1-4 Inaeleza “Injili” ni Yesu, Jinsi alivyo na kile alichokikamilisha.

Moja ya njia ya kujifunza kitu kilivyo – ni kueleza kisicho Injili. Sina kitu kizuri ninachoweza kukifikiria zaidi ya upotofu wa Wagalatia.

Historia ya Wagalatia inapatikana katika kitabu cha Matendo. Paulo anafika katika eneo ambalo kwa leo tunaliita ni Uturuki. Paulo alifundisha Injili safi ya neema, iliyokamilishwa kwa njia ya zawadi ya Mwana wake Mtakatifu Yesu. Kwa Paulo, maisha ya Kristo, Kifo, na kufufuka kunapokelewa kwa njia ya Imani na toba; haya yote yanahitajika kwa Mungu kwa ajili ya Msamaha wa dhambi.

Baada tu ya Paulo kuondoka eneo hilo lililokuwa linajulikana kama Galatia, Wakristo/ Wayahudi kutoka Yerusalemu walimfuata Paulo kwenye haya makanisa mapya, wakiwaambia watu kwamba wanapaswa kutii “sheria” zilizowekwa na wanadamu za dini zao, kama vile kutahiliwa, sheria za Kiyahudi za Kosha, kuheshimu sherehe za kiyahudi na siku. Paulo akayaita mafundisho yao kuwa ni, “Injili nyingine.” (1:6)

Hii aina ya injili potofu bado inaendelea hadi leo. Makanisa mengi na madhehebu kwa namna moja wameiharibu Injili ya kweli. Mistari ya neema na matendo ni kusudi lililorudiwa rudiwa katika waraka huu = kuwapinga “hawa ndugu wa uongo” ‘2:4, na ile Injili tofauti waliyohubiri, 1:6

Ni injili tofauti kwa sababu iliibadili Neema = 1:7

Ni Injili tofauti kwa sababu iliiua Neema = 2:21

Ni Injili tofauti kwa sababu ilimpinga Kristo =1:6

Ni Injili tofauti kwa sababu iliichafua Neema = 6:13; Warumi 6:1, 2

### **Paulo, aliyekuwa ni Myahudi mshika dini alielewa ni kwajinsi gani ilivyo rahisi kuchanganya dini na Injili**

1. Maisha ya kale ya Paulo kama Myahudi mshika dini = Mistari 1:10-14

**Zangatia:** Sauli alikuwa na shauku ya mila na destruti zake. =1:14

Hii inamanisha kwamba alikuwa na orodha kubwa ya matendo na hakujaribu kumpendeza Mungu!

Talmud= Sheria 613!!

**Matumizi:** Wakristo wa siku hizi wanaorodha yao na haujazivuka au unazo! Makanisa ya kimadhehebu yana sifa hizi za kuwa na “Injili tofauti.”

A. Mifano ya Injili isivyo:

### **1. Injili siyo falsafa inayokufanya kuwa mtu mwema.**

**Maelezo:** Injili siyo kitu cha wewe kujiimarisha. Injili siyo kuhusu wewe! Haikuimalishi, Bali itakubadilisha! Tazama **2Kor. 5:17**, badiliko hili linakufanya uwe kama Yeye.

**Matumizi:** Uwe makini na Injili iliyobadilishwa “Inayoongeza” mambo fulani katika maisha yako badala ya kumwongeza Yesu mwenyewe!

**Kielelezo:** Wale wanaohubiri” Joel Osteen” Injili ya kujisikia vizuri, wanakwambia ni Injili. Hiyo si Injili.

### **2. Injili siyo kibali cha kuingia mbinguni (Tiketi ya kuingia mbinguni)**

**Maelezo:** Wengi “Wamempokea Yesu” kwa njia ya maombi ya imani kama vile katika mikutano ya Billy Graham, wakidhani kwamba ni majumuisho ya Injili. “Niliomba, achana nayo” Nina tiketi ya kwenda!

**Matumizi:** Injili ni zaidi ya tiketi ya kwenda mbinguni; ni uvamizi wa mfalme na ufalme wake katika maisha yako.

### **3. Injili siyo mafanikio**

**Maelezo;** Tatizo liko katika kuchukua mafundisho ya Agano la kale, kuhusu Baraka na laana na kuyaleta katika kanisa la Agano jipya.

**Matumizi:** Unadhani kama wewe ni mwema, au mzuri, unapata Baraka na kama ni mbaya unapata laana.

### **4. Injili si kwa ajili ya mambo ya baadae- (maisha ya baadae)**

**Maelezo:** Wengi hawana matumaini ya nguvu iliyopo au faida ya kuokolewa kwao. Kwao Injili ni kwa ajili ya yajayo tu. Ni mbingu tu tena kwa Mungu wangu!

**Matumizi:** Injili ni ya Mungu na Ufalme wake. Tuko katika Kristo na utawala wake, ufalme na urejesho unaendelea ndani yetu sasa.

## **5. Injili siyo Upendo (Kwa Jirani yako)**

**Maelezo:** Mekanisa ya kidhehebu yanaishi kwa aina hii ya ujumbe wa uongo kuhusu upendo tu. Mpende Mungu na mpende jirani yako!

Hii ni injili nyingine kwa sababu ni vigumu kufanya! Yesu anaweza kuwapenda adui zake si wewe!